
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO

## Jarida la Robo ya Pili ya Mwaka

## (Oktoba- Desemba)

Toleo Na. 0002 07, Januari 2023



Chamwino_dc Chamwino Dc

# Yaliyomo

3 TCI yatambulisha mradi Chamwino
6 Waziri Ndugange Apongeza watumishi Hospitali ya Uhuru ,ChamwinoWizara ya
8 Mifugo na Uvuvi Yatoa Madume Bora ya ng'ombe Chamwino
12 Serikali Kufanya Maboresho Makubwa Sekta ya Mifugo na Uvuvi
14 Mkuu wa Mkoa Atoa Maelekezo kwa viongozi na Watumishi Chamwino
18 Kongamano la Vijana Kiuchumi

BODI YA WAHARIRI
Modesta Simon







*Jengo Jipya la madarasa Shule ya Sekondari Handali ambalo limekamilika, Aidha Halmasahuri ya Wilaya ya Chamwino imekamilisha vyumba 94 vya madarasa ya sekondari, Mkuu wa Wilaya Mhe. Gift Isaya Msuya, Mwenyekiti wa Halmashauri, Mhe. Edson Sweti, Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Semistatus Mashimba na uongozi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino unamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuipatia fedha Halmashauri kiasi cha Tsh. Bl. 1880,000,000/= ambazo zimewesha kukamilisha ujenzi wa madarasa haya 94 ya sekondari .*

*Watoto wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwenye Halmashauri hawatakosa vyumba vya kusomea.*



*Jengo Jipya la madarasa Shule ya Sekondari Hanet ambalo limekamilika, Aidha Halmasahuri ya Wilaya ya Chamwino imekamilisha vyumba 94 vya madarasa ya sekondari, Mkuu wa Wilaya Mhe. Gift Isaya Msuya, Mwenyekiti wa Halmashauri, Mhe. Edson Sweti, Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Semistatus Mashimba na uongozi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino unamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuipatia fedha Halmashauri kiasi cha Tsh. Bl. 1880,000,000/= ambazo zimewesha kukamilisha ujenzi wa madarasa haya 94 ya sekondari .*

*Watoto wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwenye Halmashauri hawatakosa vyumba vya kusomea .*



# Wawakilishi Shirika la Msaada La Uingereza UKAID Lafanya Ziara Chamwino



Wawakilishi wa shirika la msaada la Uingereza UKAID(FCDO) ambalo linafadhili mradi wa Shule Bora na EP4R limefanya ziara Wilayani Chamwino leo Desemba 1, 2022 kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa mradi wa Shule Bora na kupata maoni ya watendaji wa Serikali kuhusu jinsi ya kutekeleza mradi kwa ufanisi zaidi.

Katika ziara yao wametembelea makao Makuu ya Ofisi ya Halmashauri iliyopo Buigiri pamoja na shule kwa lengo la kukagua mafanikio wa mradi uliopita wa EQUIP - T.

Vilevile wamepanda miti ya mwembe kwenye eneo la Ofisi ya Halmashauri na shule ya msingi Mblenzungu kama ishara ya urafiki na ushirikiano wa dhati kati ya Serikali ya Tanzania na Uingereza.

Shule zilizotembelewa na wageni hao ni pamoja na shule ya msingi Mbelenzungu, Mnase na Msamalo.

Mradi wa Shule Bora unalenga kuiunga mkono Serikali ya Muungano wa Tanzania katika kuinua kiwango cha elimu jumuishi pamoja na kuweka mazingira salama ya kujifunzia kwa wanafunzi wote wa kike na wakiume katika shule za Serikali za Tanzania.

Kwa ushirikiano na Serikali ya Tanzania mradi huu utafanya maboresho yatakayowezesha kila mtoto kupata msingi mzuri katika elimu yakeya awali ili kuitumia fursa kwa kutoa mchangowake katika ukuaji wa nchi na maendeleo yake.

# Waziri Ndugange Apongeza watumishi Hospitali ya Uhuru ,Chamwino

Mheshimiwa Naibu Waziri OR-TAMISEMI anayeshughulikia Masuala ya afya Mhe. Festo Ndugange amefanya ziara ya kikazi Wilayani Chamwino leo Desemba 05,2022.

Katika ziara hiyo amekagua shughuli mbalimbali zinazofanyika hospitali ya Uhuru na ameipongeza wilaya kwa kupata hospitali nzuri na amewapongeza watumishi kwa kufanya kazi vizuri.

“Ni hospitari nzuri yenye miundo mbinu bora, dhamira yake ni kuona wananchi wa Chamwino na Dodoma kwa ujumla wanapata eneo bora la kupata huduma za afya. Lakini pili niwapongeze kwa usafi, kwa kweli nimeridhishwa na usafi wa hospitali, mpangilio ni mzuri na watumishi wote tupo kazini”.Amesema Naibu Waziri.

Vilevile Mhe. Waziri aliwapongeza kwa kuendelea na ujenzi wa miradi ya afya vizuri ana imani itakamilika kwa wakati ili yaanze kutoa huduma.

Alipongeza pia kwa vifaa tiba vingi ambavyo wamepewa na Serikali na katika hili aliongelea kuhusu mashine ya X - Ray ambayo imefungwa na kuanza kutumika na kusema kuwa hilio ni jambo jema ambalo litawaondolea wananchi adha ya kupatà huduma hizi mbali.

Vilevile alieleza kuwa wanajenga jengo la mtambo wa oxygen na linatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi desemba mwaka huu ili,wagonjwa watakaokuwa na mahitaji ya oxygen waweze kupata hapa pasipokulazimika kwenda hospitali ya mkoa na maeneo mengine. Lakini pia kupunguza gharama kwa wananchi.

“ kama mitambo hii ya oxygeni isipokuwepo hapa, kama mashine za xray zisingekuwepo hapa wangelazimika kwenda General hospitali ya mkoa, wangelazimika kwenda Benjamini Mkapa kwa ajili ya kupata oxygen au kupiga xray.” Amesema Mhe Ndugange.

“ Mhe. Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ameleta Chanwino mabilioni ya fedha lakini pia katika hospitali hii ya uhuru ili kuhakikisha vifaa hivi vinapatikana nawananchi wajirani wanapata huduma hapa”. Amesema Mhe. Ndugange.

Aidha ameziagiza Halmashauri zote nchini kuhakikisha zinafyata utaratibu uliowekwa na Serikali wa kutoa na kupokea dawa ili kueouka upotevu wa dawa. Vioeviie alielekeza kuhakikisha dawa zinapatikana kwa wagonjwa kwenye hisptali zote nchini kwa aslimia tisini na tano au asilimia mia moja

Mhe. Waziri aliwatia shime na kuwaekeza



kuwa Mhe. Rais abatambua kazi kubwa inyofanywa na watumishi na ndio naana amelipa stahili mbalimbali walizokuwa wanadai na bado anaendelea kulipa. Vilevile amepandisha madaraja ya watumishi kwa kiasi kikubwa na kazi hio inaendelea.

Aliwaomba watumishi waendelee kufanya kazi nakuamini kuwa serikali itaendelea kuwaboreshea mazingira yakufanyia kazi. Aliomba wawe ba lugha nzuri kwa wagonjwa.

Kuhusu suala la gari la wagonjwa Mhe Waziri aliahidi kulishughulikia kwenye magari 300 ambayo Mhe Rais ametoa fedha yanunuliwe mojawapo litapelekwa hosp wanaiali ya Uhuru na nagari hayo yanatarajiwa kuwa yamefika mwishoni mwa mwezi desemba 2022 au mwanzoni mwa mwezi januari 2023.

“Hospitali hii ni kubwa na ipo barabarani naajali zibaweza kutokea wakati wowote na ndio maana wanefunga digital xray na hivyo awahakikishie OR - TAMISEMI wataieta gari ka wagonjwa.” Amesema Mhe. Ndugange.

Kuhusu miundo mbinu alisema Serikali itaendelea kujenga majengo ambayo hayapo ili hospitali iweze kutoa huduma zinazotarajiwa.

Naye mganga mjuu wa mkoa dkt. Best Magoma alimshukuru Mhe. Waziri na kuahidi kutekeleza yote yaliyoagizwa na Mhe Naibu Waziri.



# Wizara ya Mifugo na Uvuvi Yatoa Madume Bora ya ng'ombe Chamwino

"Mifugo tuliyonayo ni mingi , ng' ombe peke yake tulionao ni ml. 35.3, kwa Afrika sisi ni wa pili kwa kuwa na ng'ombe wengi baada ya Ethiopia. Tunautajiri mwingi ambao umejificha ndani yetui ni lazima kuubadilisha ili uweze kubadilisha maisha ya Watanzaniana kuondokana na hali duni. Na ndio maana wao kama wizara ya mifugo wamekuja na mpango wa mabadiliko".

Maneno hayo yamesemwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki alipokuwa kwenye hafla ya ugawaji wa madume bora kwa vikundi vya wafugaji iliyofanyika Wilayani Chamwino Novemba 24, 2022 katika viwanja vya Ofisi ya kilimo.

Ameeleza kuwa lengo la kufanya mabadiliko makubwa kwenye sekta ya mifugo ni kutokana na kuwa na mifugo yenye tija ndogo. Ng'ombe wanauzito kidogo na wanatoa maziwa kidogo..

"Tunafunga kiasili ufugaji ambao hausaidii sana kuchechemua uchumi

wetu na uchumi wa kaya”. Alisema Mhe. Waziri Mashimba.

‘Masoko tuliyonayo ndani na nje hayahitaji aina ya mifugo tuliyonayo na hasa nyama. Nyama inahitajika na soko la Ulaya, China”.

Alieleza kuwa wanaviwanda vya kusindika nyama lakini havina malighafi, hivyo shughuli hii ni mojawapo ya kutekeleza maboresho ya sekta ya mifugo na wameamua kufanya maboresho makubwa matatu.

Jambo la kwanza ni uhamilishaji wa koo safi na tayari wameahanunua mtambo mkubwa kwa ml. 600 walizopewa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan na uhimilishaji utafanyika nchi nzima. Na ng’ombe hao waliofanyiwa uhamilishaji watakuwa na uwezo wa kuwa na kilo 150 hadi 200 kwa ng’ombemmoja.

Jambo la pili katika maboresho ni kugawa madume bora ambayo yatasaidia kusaidia kubadilisha ng’ombe waliopo sasa. Alieleza madume wanayoyagawa ni madume ya nyama na baadae watagawa madume kwa ajili ya maziwa. Uzinduzi huu utakuwa ni kwa nchi nzima .

Aliendelea kueleza kuwa ng’ombe hawa watakuwa na uwezo wa kuzalisha maziwa kati ya lita 5 hadi 10 kwa ng’ombe mmoja. “Maziwa yatakayozalishwa kwa ng’ombe mmoja ni kati ya lita 5 hadi 10 kwa ng’ombe mmoja.

Maboresho ya tatu yaliyoelezwa ni njia ya kunenepesha mifugo na bl.4.4 zimetengwa kwa ajili ya unenepeshaji kwenye vituo atamizi ambavyo wamepewa vijana. Kwa kufanya hivyo watawatengenezea ajira vijana. Vilevile alieleza kuwa kwa kufanya hivyo pia watabadilisha akili ya wafugaji. Kupitia vijana hao wafugaji wataweza kubadili fikra zao.

Madume yaliyogawiwa kwa vikundi vya wafugaji ni 50 na kila moja linauwezo wa kupanda majike 25 na linauwezo wa wa kupanda kwa miaka minane.

Ilielezwa kuwa madume hayo wameyagawa bure kwa wafugaji lakini serikali imeyanunua kwa gharama kubwa, dume moja limenunuliwa kwa shilingi ml.2.5, hivyo aliomba watakaogawiwa wayatunze.

“Watakaogawiwa watunze madume haya, yanahitaji kuogeshwa ili yasipate kupe na hayatakiwi kuchungwa.Wanapewa bure lakini Serikali haikuyapata bure, dume moja limenunuliwa shilingi ml.2.5”. Alisema Mhe. Waziri.

Aidha aliwaelekeza kuwa wasiwe wachoyo kama wanamajike machache wampe mwenye majike mengi.

Naye mwalilishi wa mbunge jimbo la Chamwino ambaye ni Katibu wake ndugu Muhsini Mulokozi pamoja na mwenyekiti wa wafugaj ndugu John Kochochoi walimshukuru Mhe. Waziri kwa madume hayo na kumuomba amfikishie shukrani zo kwa Mhe. Rais Mama Samia Suluhu Hassan. Aliahidi kusimamia na kuyatunza madume hayo waliyopewa.

Naye Mkuu wa wilaya ya Chamwino Mhe. Gift Isaya Msuya alishukuru kwa kupata madume hayo na kuahidi kuwa hayatauzwa na watasimamia wafugaji waweze kuyatunza na alisisitiza wafugaji wasiwe wachoyo bali waende wakawape na wengine.

# Kikundi cha Vijana Buigiri Chapewa Vitendea kazi




Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino Dkt. Semistatus H. Mashimba amekabidhi mashine ya kukatia na kuchomelea vyuma Novemba 14, 2022 kwa vijana wa kikundi cha WASAKA TONGE Kata ya Buigiri ambayo imetolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na watu wenye Ulemavu.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo amewataka vijana hao kupitia mashine hiyo inabidi wazalishe zaidi ya wanavyozalisha sasa. Aliwapongeza kwa kupata mashine hiyo na kuwa mfano bora kwa Wilaya yachamwino. Kufanya kazi kwa ushirikiano kama kikundi kinawapa matumàini Serikali.

kuhusu changamoto ya bei waliyoitoa alieleza kuwa hilo siyo tatizo kwani uanisababisha wewe mwenyewe kutokana na bidhaa unayoizalisha hivyo aliwashauri kuzalisha bidhaa bora na kuongeza gharama kwa jinsi bidhaa alizozalisha. Hivyo ongezeko la bei litumike kama fursa.

Alielekeza Afisa Maendeleo ya jamii Wilaya kuhakikisha anasimamia vijana hao kupata tenda kwenye miradi mbalimbali inayotekelezwa na Halmashauri.

“Afisa maendeleo simamieni vijana hawa wapeni tenda kwenye miradi ya Halmashauri ili waweze kujiimarisha zaidi na ninyi mfanye kazi usiku na mchana ili muweze kukamilisha hayo mahitaji.” Alisema Dkt. Mashimba.

Naye Diwani wa kata ya Buigiri Mhe. Keneth Yindi amewaeleza vijana kuwa wanayobahati kupata mashine hiyo kwani ni Halmashauri chache sana zilizopewa mashine hizo na wao wakiwemo. Ameeleza kuwa ni Halmashauri 52 tu kwa nchi nzima na kwa mkoa wa Dodoma ni Halmashauri 3 tu ndizo źimeweza kupata mashine.




# Maeneo Sita Kufanyiwa Maboresho Sekta ya Mifugo na Uvuvi

Wizara ya mifugo imepanga maeneo sita ya kuyafanyia maboresho. Hayo yamesemwa na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na uvuvi Ndugu Tickson Nzunda alipokuwa akizungumza kwenye ufunguzi wa mafunzo rejea kwa maafisa ugani Nchini.

Mafunzo hayo yameanza kufanyika Novemba 14, 2022 Wilayani Chamwino na yatafanyika kwa siku mbili.

Maeneo yaliyopangwa ni pamoja na afya ya mifugo ambapo jukumu walilonalo ni kuhakikisha mifugo inakuwa na afya bora. Pia alieleza kuwa jambo la kuchanja mifugo na kuogesha mifugo ni lazima.

“Jukumu letu kuhakikisha mifugo inakuwana afya bora Kitaifa na Kimataifa.” Alisema Katibu Mkuu.

Aidha alieleza kuwa Wizara imegawa dawa ya ruzuku, na mikoa yote imepata. Kwa kufanya hivyo wataweza kudhibiti magonjwa. Alisisitiza sheria, kanuni na taratibu za ufugaji bora ni lazima zizingatiwe.

Kuhusu kuimarisha huduma za ugani za mifugo alisema hilo ni jambo la lazima na ni lazima kuwe na mfumo wa utendaji wa wenye matokeo.

Jambo jingine lililopangwa ni kuimarisha suala la masoko kwa kuimarisha minada. Kuhakikisha mapato ya Halmashauri na Serikali yanapatikana.Aliongeza kuwa wafugaji ni lazima wachangie kwenye sekta ya mifugo.

Kwenye suala la malisho Katibu Mkuu alieleza kuwa ni lazima wafugaji waone juwa wanawajibu wa kupanda malisho. Serikali itaanzisha mashamba darasa ya malisho na kuwapa elimu wafugaji.

Jambo jingine ni kuimarisha ushirikishwaji wa huduma za ugani kwa sekta binafi na wafugaji wenyewe.

Vilevile wataimarisha mashamba ya Serikali ili yawe na mifugo bora na kuyafanya yawemya kibiashara. “Tujengeane uwezo ili kufuga kibiashara.” Alisema Katibu Mkuu.

Kuimarisha ranchi za Kitaifa ili kudhibiti ufugaji holela. Wafugaji washirikiane na Halmashauri ili kupata maeneo ya kufugia kwa lengo la kufuga kibiashara.

# Serikali Kufanya Maboresho Makubwa Sekta ya Mifugo na Uvuvi



“Serikali ya awamu ya sita imepanga kufanya mabadiliko makubwa kwenye sektamya mifugo.”

Hayo yamesemwa kwenye ufunguzi wa mafunzo rejea kwa maafisa ugani Nchini kwa kanda ya kati yanayofanyika Wilayani Chamwino kwa siku mbili, Novemba 14,2022.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo Waziri wa mifugo na uvuvi Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki amesema sekta ya mifugo inawategemea maafisa ugani katika kuleta matokeo chanya japokuwa wapo wachache. Alieleza kwa uchache wao huohuo kama watakipenda wanachokifanya watafanikiwa.

“ Sekta ya mifugo kwa matokeo chanya tunawategemea ninyi. Ninyi ndio askari wa mstari wa mbele ili kuleta mafanikio.” Alisema Mhe. Ndaki.

“Kwa mpango huu wa mabadiliko tunaweza kuleta mabadiliko ya mtu mmoja mmoja. Aliongeza kusema kuwa sekta ya mifugo kwa kiasi kikubwa imetawaliwa na ufugaji wa asili na tukiendelea na na tukiendelea na uasili huu hautatufikisha mahali pazuri.” Alisema Mhe. Ndaki.

Aidha Mhe. Waziri Ndaki alieleza kuwa kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022 sekta ya mifugo inakuwa kwa 7% . Aliendelea kusema kwa idadi ya mifugo tuliyonayo tungefuga kwa tija tungeweza kuishi kwa kutegemea ng’ombè tu. Lakini kwa sasa unakuta ng’ombe wanauzito mdogo jambo linalopelekea kuwa na tija kidogo na maziwa machache.

Mhe. Ndaki alieleza kuwa kwa mwaka huu wa fedha wamepanga kufanya nafunzo kwa ngazi zote kwa wataalamu na wafugaji. Alisema tukiwaelimisha wafugaji wetu itakuwa chanzo cha kuwabadilisha ili wafuge kwa tija.

Vilevile Mhe. Waziri alieleza kuwa kupitia mpango wa maboresho wameanzisha vituo atamizi kwa vijana ambapo vijana 240 waliohitimu masuala ya mifugowamesajiliwa kwenye vituo hivi. Lengo likiwa ni kutengeneza wafugaji wa leo na kesho ili kuwa na wafugaji wenye tija.

Alieleza kuwa wanamshukuru Mhe. Rais mama Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia bl. 5 kuwezesha vituo hivyo na mradi huo wameuita “Samia Ufugaji Programme”. Baada ya mwaka mmoja watafuzu na kuondoka na kuita watu wengine.

Kuhusu changamoto ya vitendea kazi Mhe. Ndaki alieleza kuwa tayari wameshagawa pikipiki 300 na kwa mwaka huu wa fedha watatoa pikipiki 1200 na magari 13 kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa.

Katika kufikia maboresho Wizara imeanzisha mfumo ( M - kilimo na Ugani kiganjani) ambayo itawezesha Wizara kupokea taarifa moja kwa moja toka kwa maafisa ugani na alitoa rai kwa ambao hawajajisajili wajisajili. Aliagiza wafugaji pia wasajiliwe kwenye mfumo.

“Tumeanza mifumo ya usimamizi wa huduma za mifugo ( M - kilimo na ugani kiganjani) kupitia mifumo hii Wizara itapata taarifa moja kwa moja toka kwenu.” Alisema Mhe. Waziri.

# Mkuu wa Mkoa Atoa Maelekezo kwa viongozi na Watumishi Chamwino



Mkuu wa Mkoa ametoa maelekezo mbalimbali kwa watendaji wa Serikali ikiwemo suala la Elimu ambapo alisema bado ufaulu wa mkoa upo chini, upungufu wa miundo mbinu, utoro, mimba mashuleni na wanafunzi kuolewa wakiwa bado mashuleni.

Maelekezo hayo ameyatoa alipofanya ziara ya kikazi Wilayani Chamwino Novemba 10, 2022 iliyokuwa na lengo la kuzungumza na viongozi hao na watumishi pamoja na kukagua miradi ya maendeleo.

Aliwataka wadau wote wa elimu wafanye vikao kuanzia ngazi ya kata hadj wilaya na kufanya tathimini kuhusu elimu kwenye maeneo yao. Aliwataka viongozi kuongea na wananchi kuhusu kuunga mkono ujenzi wa miundombinu ya shule kwani Serikali imeshafanya sehemu kubwa.

Kuhusu kilimo mkuu wa mkoa ameelekeza kipewe kipaumbele na kukiwekea mikakati mizuri kwani 72% ya wananchi ni wa kulima. Alisema Mhe. Rais Mama Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa kwenye kilimo, alitolea mfano pikipiki zilizotolewa kwa maafisa ugani nchi nzima pamoja na miradi mingine ikiwemo ya umwagiliaji na hivyo wanamshukuru sana. Alisisitiza maafisa ugani wasimamiwe.

Vilevile Mkuu wa Mkoa alisisitiza kuhusu suala la uwajibikaji kwa watumishi wa umma ili kuleta matokeo yenye tija kwani Serikali imewekeza fedha nyingi kwenye mishahara ya watumishi.

“Watumishi Serikali inatuthamini sana na ndio maana inatulipa mishahara. Fedha nyingi imewekwa kwenye mishahara, hivyo ni lazima tuwajibike kwani Serikali inatutegemea tulete tija.”

Kuhusu utawala bora alielekeza vikao vyote vya kisheria vya kijij na kata viwe vinafanyika na agenda ziwe zinazotakiwa. Kusimamia maadili ya watumishi. Taarifa za miradi zitolewe kwa wananchi. Kusikiliza kero za wananchi ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kupokea kero hizo.

Mkuu wa mkoa pia alitembelea mradi wa shamba la zabibu Chinangali wenye hekari 6000 ambao unatarajiwa kuanza upandaji hivi karibuni.

# Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Atatua Kero Chamwino



Mkuu wa mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Sitaki Senyamule amefanya ziara ya kikazi wilayani Chamwino, Novemba 10, 2022 kwa lengo la kuzungumza na viongozi mbalimbali ngazi ya wilaya pamoja na watumishi na kukagua miradi ya maendeleo.

Akiwa kwenye kikao na viongozi hao pamoja na watumishi kilichofanyika kwenye jkumhi wa mikutano wa Halmashauri Mkuu wa Mkoa alipokea kero mbalimbali na zote zilipatiwa majibu.

Hoja zilizowasilishwa na kupatiwa majibu ni pamoja na soko la zabibu kusuasua na kuwa na bei ya chini na baadhi ya wakulima kutolipwa fedha zao mpaka sasa, ambapo majibu yalitolewa kuwa Serikali imeshaanza kulitafutia ufumbuzi suala la soko la zabibu.

Ilielezwa kuwa kwa mwaka huu wa fedha Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kujenga kiwanda kwa ajili ya kukamua mchuzi wa zabibu ikiwa ni pamoja na kujenga matenki ya kuhifadhia mchuzi wa zabibu suala ambalo litapunguza adha hiyo.

Kuhusu suala la wakulima kutolipwa fedha zao ilielezwa kuwa tayari kampuni ya jambo wanaendelea kulipa na walichelewa kulipa kutokana na suala hilo la kununua kutokuwa kwenye mpango wao wa bajeti isipokuwa walifanya hivyo baada ya kuombwa na Serikali kununua zabibu ili kunusuru zisiharibikie shambani.

Kero nyingine ilikuwa ni kuhusu bwawa la Manchali ambalo limechimbwa tangu mwaka 1997 na tangu kipindi hicho halijawahi kufanyiwa ukarabati na tayari limejaa mchanga na kufanya shughuli za umwagiliaji kushindwa kufanyika.

Akijibu hoja hiyo Mkuu wa Idara ya Kilimo ndugu Godfrey Mnyamale alieleza kuwa bwawa hili limeshaandikiwa maandiko na WFP walielekeza uongozi wa kata kutunza mazingira ya bwawa na kutoruhusu mifugo kuingia na kuchunga kwenye eneo la bwawa na iwapo hayo yatatekelezwa kwenye bajeti ya 2023/2024 wataleta fedha kwa ajili ya kurikarabati.

“Wameshaandika maandiko, WFP walielekeza uongozi wa kata kusimamia kutunza mazingira ya bwawa na kutoingiza mifugo na bajetimya 2023/2024 wataleta fedha.’ Alisema Mnyamale.

Kuhusu kero ya daraja la Chilonwa ambalo limesababisha ajali nyingi kipindi cha masika, afisa kutoka TANROAD alieleza kuwa kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha wa 2022/2023 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya usanifu na kazi hiyo ya usanifu ambayo inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Februari 2023, watatangaza tenda ya ujenzi wa daraja.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma Bibi Fatuma Mganga ameipongeza Halmashauri kwa kupata mradi wa bwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na ameielekeza Halmashauri kuweka mipango mizuri ili kuongeza mapato.

“Nawapongeza kwa kupata fursa za mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Natarajia katika mradi wa bwawa mlioupata mipango iwe mizuri ili kuongeza mapato.”Alisema Katibu Tawala Mkoa.



# Madiwani waaswa Kusimamia Amani



Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Mhe. Gift Isaya Msuya ametoa rai kwa Wahe. Madiwani kuhakikisha wanachukua tahadhari dhidi ya mambo madogo madogo ya uvunjifu wa amani kwenye maeneo yao. Ameyasema hayo kwenye kikao cha Baraza la Madiwani Novemba 8, 2022. Alieleza kuwa iwapo atatokea mtu anataka kuharibu amani taarifa itolewe ili aweze kuchukuliwa hatua.

“ Ni vema tukachukua tahadhari ya mambo madogo madogo ya uvunjifu wa amani kwenye maeneo yetu. Tukionamtu yeyote anataka kuharibu amani, tulitolee taarifa suala hilo ili achukuliwe hatua.” Alisema Mkuu wa Wilaya.

Alieleza pikuwa kuna baadhi ya viongozi wanaoongoza migomo na maandamano na kusema Serikali haiongozwi kwa mihemuko. Aliongeza kusema kuwa Serikali tayari imeanza kuchukua hatua kwa viongozi hao

Vilevile Mkuu wa Wilaya alisisitiza kuhusu suala la ukusanyaji wa mapato kwani fedha zinahitajika kupelekwa kwenye miradi ya maendeleo, na kueleza kuwa Mkuu wa Mkoa ametoa maelekezo kwa kila Halmashauri kuhakikisha inakusanya kwa 100%. Alieleza kuwa Madiwani wakiamua hawawezi kushindwa kukusanya kwa 100%.

“ Maelekezo ya Mkuu wa Mkoa hangependa Halmashauri ikusanye chini ya 100%.” Alisema Mkuu wa Wilaya.

Aidha Mkuu wa Wilaya alitilia mkazo kuhusu suala la kukamilisha miradi ya ujenzi wa madarasa kwa wakati kulingana na muda wa kukamilisha uliowekwa na mkoa wa tarehe 31, Novemba 2022.

Alisisitiza pia kuhusu suala la umoja na mshikamano kwani maendeleo wanayoyafanya ni kwa ajili ya manufaa ya wananchi. Aliomba kila mmoja afanye kazi kwenye mipaka yake na kuwe na kuheshimiana.

# Kongamano la Vijana Kiuchumi



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, vija, Ajira na wenye Ulemavu, Mhe. Patrobas Katambi amewataka vijana kuzitumia fursa zinazotolewa na Serikali ili kujiletea maendeleo katika mazingira wanayoishi.

Akizungumza katika kongamo la vijana lilifonyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino 28, Oktoba 2022, amesema wajibu walio nao Ofisi ya Waziri Mkuu wanaojihusisha na ajira kwa vijana kuwa wanahakikisha wanabadilisha mtazamo kwa vijana.



Mhe. Katambi amesema Serikali ina wajibu wa kutimiza yale yanayotakiwa kwa vijana na wanapaswa kufanya mambo ambayo yatawaletea manufaa baadaye.

"Wajibu mkubwa tulionao Ofisi ya Waziri Mkuu wanaoshughulika na masuala ya vijana ni kuhakikisha tunabadilisha mitazamo na tuwe na mitazamo chanya kwa vijana na kubadilisha mitazamo, fikra sio jambo rahisi".

"Kwamba Serikali inatengeneza mazingira wezeshi ya kuwasaidia vijana na kuhakikisha wale vijana ambao wako kwenye masuala ya kujikwamua kiuchumi inaweka progamu mbalimbali pia kijana fanya mambo ambayo jamii itakuelewa baadaye na hatakama sio baadaye itaelewa kwa mambo mema unayofanya," amesema.

Katambi amesema vijana wanapaswa kufuatilia na kujua utaratibu wa kujipatia mikopo kupitia fungu linalotengwa na Serikali kupitia Afisa maendeleo ya vijana na Afisa maendeleo ya Jamii ambao wapo kwenye maeneo yao ya Halmashauri ili kujikwamua kiuchumi

Hata hivyo amesema vijana wanapaswa kujiunga na vikundi ili waweze kupata mikopo hiyo na kuzitumia kwa malengo endelevu katika jamii

Amesema pia Serikali imeweka mpango wa mikopo kwa ajili ya elimu ya juu.

"Serikali imeanzisha sheria nyingine ya fedha za Halmashauri ambapo kutakuwa na mgawanyo wa asilimia kumi (10%) ya mapato ghafi ya Halmashauri, asilimia kumi (10%) kila mwaka zitengwe kwaajili ya shughuli za vijana, kwa vijana tunapata asilimia nne (4%), kwa wanawake asilimia nne (4%) na kwa watu wenye ulemavu asilimia mbili (2%) na sharti ni kwamba mjiunde katika makundi ya vijana kumi (10) ili mpewe fedha hizo na zimekuwa zikitoilewa nchini kote.

"Ni wewe tu kufuatilia fursa na kuweza kupata taarifa rasmi kupitia Afisa maendeleo ya vijana na Afisa maendeleo ya Jamii ambao wapo kwenye maeneo yetu, fedha zinatolewa lakini changamoto pia imekuepo hatuzi tumii vizuri au hatuhamasiki kwenda lakini pia vijana hatujitokezi kwenda kujiunga kwenye vikundi, sasa hapo ni kwa aliye soma na siyesoma Serikali imekuwekea mpango," amesema.

# Wafugaji Chamwino watakiwa Kushiriki Upimaji wa Maeneo yao



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino Dkt.Semistatus H. Mashimba, amewataka wafugaji kushiriki katika zoezi la upimaji wa maeneo yao ili kuondokana na migogoro inayojitokeza katika jamii.

Akizungumza katika mkutano na wafugaji wa Wilaya ya Chamwino Oktoba 19, 2022, amesema lengo la zoezi hilo ni kusaidia kuondoa migogoro kati ya wafugaji na wafugaji, wakulima na wafugaji katika maeneo yao.

Vilevile amewaelekeza wafugaji kuwa wanapaswa kutunza nyaraka walizo nazo ili kupata taarifa za uhakika wakati wa utekelezaji wa zoezi hilo.

Amesema Serikali inatengeneza miongozo mizuri kupitia zoezi hilo ili kutekeleza miradi ya josho kwaajili ya mifugo.

Aidha amewaasa wafugaji hao kuchangia gharama za upimaji wa maeneo yao.

Kwa upande wa Wafuagji wamesema wapo tayari kutoa ushirikiano ili kuepusha migogoro na kuweza kutambua mipaka yao.

Amesema zoezi hilo linatarajiwa kutekelezwa kwa siku 20 na linakusudiwa kuanza tarehe 24 Mwezi huu.

“zoezi hili litaanza mapema iwezekanavyo na natarajia ndani ya siku 20 liwelimekamilika na zoezi hili rasmi litaanza tarehe ishirini na kukamilika kwa siku hizo”.

“Naomba kupata ushirikiano kutoka kwenu ili tuweze kutekeleza jambo hili kwa haraka zaidi, na jambo hili litasaidia kuondoa migogoro katika mazingira yetu tunayo ya ishi kama vile migogoro kati ya wafugaji na wafugaji pia wafugaji na wakulima,” amesema Dkt. Mashimba.

Wamesema kila mfugaji alijinunulia eneo kwa ajili ya shughuli za ufugaji na zoezi hilo likikamilika litakuwa mfano kwa Wilaya zote za nchi ya Tanzania.

“Haya maeneo ni ya kwetu tunaomba tukapimiwe kwa haraka na jambo hili la upimaji litasaidia kuondokana na changamoto za kuingiliana katika mipaka yetu”.

“Pia zoezi hili likikamilika litakuwa mfano wa kuigwa kwa Halmashauri zote za nchi yetu ya Tanzania”, wamesema.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - TAMISEMI

# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO

## TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino Dkt. Semistatus Mashimba anautaarifu umma kuwa Halmashauri imepokea kiasi cha Tsh. 890,000,000 fedha kutoka Serikali Kuu mwezi Oktoba 2022 kwaajili ya miradi ya maendeleo ya sekta ya Elimu na Afya

| NA | JINA LA MRADI | IDADI | AINA YA MRADI | JINA LA KITUO | MAPOKEZI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Zahanati | 1 | Zahanati | Ilolo | 50,000,000 |
| 2 | Ujenzi wa Zahanati | 1 | Zahanati | Msamalo | 50,000,000 |
| 3 | Ujenzi wa maabara | 1 | Sekondari | Mvumi Mkaulu | 50,000,000 |
| 4 | Ujenzi wa maabara | 1 | Sekondari | Majeleko | 30,000,000 |
| 5 | Ujenzi wa maabara | 1 | Sekondari | Makang'wa | 50,000,000 |
| 6 | Ujenzi wa maabara | 1 | Sekondari | Mvumi misheni | 50,000,000 |
| 7 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 | 10 | Shule shikizi | Bwawani | 11,000,000 |
| 8 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 | 10 | Shule shikizi | Mbugani | 11,000,000 |
| 9 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 | 10 | Shule shikizi | Chiteleche | 11,000,000 |
| 10 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 | 10 | Shule shikizi | Chitolomelo | 11,000,000 |
| 11 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 | 10 | Shule shikizi | Kikoti | 11,000,000 |
| 12 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 | 10 | Shule shikizi | Maumi | 11,000,000 |
| 13 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 | 10 | Shule shikizi | Mbelezungu | 11,000,000 |
| 14 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 | 10 | Shule shikizi | Mchoya | 11,000,000 |
| 15 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 | 10 | Shule shikizi | Mizengo pinda | 11,000,000 |
| 16 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 | 10 | Shule shikizi | Nyarendeka | 11,000,000 |
| 17 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 | 10 | Shule shikizi | Lugala | 11,000,000 |
| 18 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 | 10 | Shule shikizi | Mhonvu | 11,000,000 |
| 19 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 | 10 | Shule shikizi | Wali | 11,000,000 |
| 20 | Ujenzi wa vyoo matundu 10 | 2 | Shule shikizi | Matembe | 11,000,000 |
| 21 | Ujenzi wa nyumba ya mwalimu two in one | 2 | Shule shikizi | Mbelezungu | 50,000,000 |
| 22 | Ujenzi wa nyumba ya mwalimu two in one | 2 | Shule shikizi | Matembe | 50,000,000 |
| 23 | Ujenzi wa nyumba ya mwalimu two in one | 2 | Shule shikizi | Mbugani | 50,000,000 |
| 24 | Ujenzi wa nyumba ya mwalimu two in one | 2 | Shule shikizi | Mwaumi | 50,000,000 |
| 25 | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa | 2 | Msingi | | 40,000,000 |
| 26 | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa | 2 | Msingi | | 40,000,000 |
| 27 | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa | 2 | Msingi | | 36,000,000 |
| 28 | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa | 2 | Msingi | | 40,000,000 |
| 29 | Ukamilishaji wa ujenzi wa mabweni | 1 | Sekondari | Manchali | 20,000,000 |
| 30 | Ujenzi wa uzio wa Bweni shule maalum | 1 | Msingi | | 60,000,000 |
| 31 | Ukamilishaji wa ujenzi wa Bweni | 1 | Msingi | Majeleko | 20,000,000 |
| Jumla | | 166 | | | 890,250,000 |

Chamwino Dc    Chamwino_dc    www.chamwinodc.go.tz




# Foundation for disabilities watoa msaada Chamwino

Taasisimya Foundation for Disabilities mkoa wa Dodoma imekabidhi vifaa kwa ajili ya walemavu wasioona pamoja na wenye ulemavu wa ngozi.

Makabidhiano hayo yamefanyika Ofisini kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Dkt. Semistatus H. Mashimba, leo Desemba 12, 2022.

Akizungumzawakatiwamakabidhiano hayo ndugu Maiko Salali amesema vifaa vilivyokabidhiwa ni mashine ya kuandikia wasioona yenye thamani ya shilingi milioni mbili na fimbo kwa ajili ya wasioona, pamoja na mafuta kinga kwa ajili ya wenye ulemavu wa ngozi zaidi ya chupa mia moja. Aidha wameahidi kuendelea kuleta vitu hivyo kadiri watavyokuwa wanavipata.

Mkurugenzi Mtendaji amewashukuru wawakilishi wa Taasisi hiyo kwa msaada wao kwa kuwatambua watu wenye ukemavu wa wilaya ya Chamwino. Akiwahakikishia kuendeleza ushirikiano uliopo jati yao na kuahidi na vifaa wakivyovikabidhi vitakuwa salama na vitafika kwa walengwa

# TCI yatambulisha mradi Chamwino

Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kwa kushirikiana na wadau wa TCI wakishilikiana na Jhpiego wametambulisha mradi utakaohusumasuala ya uzazi wa mpango.

Mradi huu umezinduliwa Desemba 13, 2022, kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino.

Mradi huu umetambulishwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Chamwino pamoja na Wakuu wa Idara wa Halmashauri.

Akizungumza katika kikao hicho Mkurugenzi wa shirika la Jhpiego Tanzania Bibi Rose Mzava anesema mradi huu unatekeoezwa katika mikoa nane Nchini ukiwemo mkoa wa Dodoma. Kwa mkoa wa Dodoma walianza na Halmashauri ya jiji la Dodoma na sasa wanaanzisha Chamwino.

Akizungumza alipokuwa anafungua kikao nwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ndugu Mohamed Mfaki amesema wameupokea mradi huo kwa asilimia mia moja. Aliwaomba wakuu wa Idara kutoa ushirikiano na kuyapokea maelekezo yatakayotolewa kwa umakini ili mradi uwe na tija.

Vilevile aliwaomba kupekeka elimu kuhusu mradi huu kwa wananchi pamoja na kupeleka !huduma rafiki kwa vijana.

Kwenye utambulisho huo wajumbe waliweza kujadili na kuuliza maswali mbalimbali kuhusu mradi na maswali yote



Naye Mratibu wa mama na mtoto (RCH) wa Halimashauri ya jiji la Dodoma alitoa ushuhuda wa jinsi wanavyotekeleza mradi huo kwenye Halmashauri yao na mafanikik ambayo tayari wameyapata.

Mwisho wajumbe waliombwa na Bibi Mfalila msimamizi wa mradi kwa mkoa wa Dodoma kujitokeza kwa hiari kwa ajili ya kuwa ma ‘focal person’ wa mradi ambapo walijitokeza watumishi watano, Hàppy Mgongo kutoka Idara ya Elimu msingi, Raymond Mahugi kutoka Idara ya Mipango, Zena Ibrahim kutoka Idara ya Usafi na udhubita wa taka, Nicholaus Achimpota kutoka idara ya utamaduni, saana na michezo na Mtemela kutoka Idara ya Ujenzi

HALMASHAURI YA WILAYA

CHAMWINO


Chamwino Buigiri

Chamwino Dc

Chamwino_dc

www.chamwinodc.go.tz

S.L.P 1126 Dodoma